



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ZOEZI LA
UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA
WAPIGA KURA

Dar es Salaam, 10 Januari, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina jukumu la kuandikisha Wapiga Kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Hivi sasa Tume iko katika utekelezaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Uboreshaji huu unawahusu Raia wa Tanzania ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wale ambao watatimiza umri wa miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2020. Pia, unahusisha wale ambao wamehama kutoka maeneo yao ya awali na kuhamia maeneo mengine ya uchaguzi na wale ambao Kadi zao zimeharibika au kupotea. Zoezi la uboreshaji pia linajumuisha kuwaondoa wale ambao wamepoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari, mathalan waliofariki.

Uboreshaji wa Daftari umegawanyika katika *Routes* ambapo zoezi hufanyika kimikoa kwa awamu. Tangu kuzinduliwa kwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mnamo tarehe 18 Julai, 2019 mkoani Kilimanjaro, tayari zoezi limekamilika kwenye mikoa ishirini na tano (25), halmashauri za wilaya 146 na majimbo 205 Tanzania Bara na Zanzibar. Mikoa hiyo kwa Tanzania Bara ni pamoja na Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu, Mara, Mwanza, Kigoma, Tabora, Songwe, Kagera, Geita, Shinyanga, Katavi, Rukwa, Singida, Dodoma, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma na Tanzania Zanzibar mikoa ya Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi.

Hivi sasa Tume inajiandaa kuanza zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara. Tayari Mikutano na Wadau wakuu wa Uchaguzi imefanyika na elimu na hamasa kwa Wananchi inaendelea kutolewa. Zoezi hili litafanyika kwa siku saba (7) kuanzia tarehe 12 hadi 18 Januari, 2020.

Awamu zilizobaki katika ukamilishaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari zinajumuisha mikoa ya Tanga na Morogoro (Halmashauri za Mji wa Ifakara, Wilaya ya Malinyi na Ulanga) ambapo zoezi litafanyika kuanzia tarehe 23 hadi 29 Januari 2020, Mkoa wa Morogoro (Halmashauri za Manispaa ya Morogoro, Wilaya ya Gairo, Kilombero, Kilosa, Morogoro na Mvomero) kuanzia tarehe 03 hadi 09 Februari 2020, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es salaam kuanzia tarehe 10 hadi 16 Februari 2020.

Mchakato wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa awamu ya kwanza utahitimishwa kwa Uwekaji Wazi wa Daftari ili kutoa fursa kwa Wananchi kuhakiki taarifa zao zilizomo kwenye Daftari.

Imetolewa na:



Dkt. Cosmas Mwaisobwa

Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI